# Kristo 4



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.


SIO MDA MREFU BAADA YA ISHARA YA KWANZA YA YESU, ALIENDA MASHAMBANI MWA YUDEA.
WATU WALIANZA KUMFUATA. KUMSIKILIZA.
NA WAFUASI WAKE WALIWABATIZA WENGI WALIOMFUATA.
WAWEZA KUAMINI HILI?
NAJIHISI... SIFAI...
KAZI YA YESU ILIANZA KIRASMI.
NA HAIKUWA SIRI.
WAONAJE HAPA?
SIJUI! CHA MUHIMU, YOHANA YWAFKIRIA NINI KULIHUSU?
UPANDE WA PILI WA MTO YORDANI . . .
MWALIMU! MWALIMU!
NAAM, NAAM, KUNA NINI?
NI MWANAMUME ULIYEMBATIZA TULIPOKUWA UPANDE MWENGINE WA MTO YORDANI!
ANBATIZA SAA HIZI, MWALIMU!
KILA MMOJA AENDA KWAKE BADALA AJE KWAKO!
UTAFANYAJE?
NTAFANYAJE MUELEWE?






MARKO 1:4; MATHAYO 4:12; LUKA 3:19-20




MARKO 1:4; MATHAYO 4:12; LUKA 3:19-20


BWANA. UMEWATIA WAFARISAYO WASI.
HAWAPENDI MAFUNZO YAKO WALA YANAVYOHUSIANA NA YOHANA.
SANA SANA KWA KUWA YOHANA AMEKAMATWA NA MFALME!
AMEKAMATWA NA HERODE.
NABII HAESHIMIWI KWAO NYUMBANI.
LABDA NI WAKATI WETU KUENDELEA NA SAFARI TURUDI ZETU --
"-- KUELEKEA GALILAYA."
SAFARI YAO ILIWAPELEKA SAMARIA NA SYCHAR AMBAKO VIZAZI VILIVYOPITA YAKOBO ALIMPA MWANAWE YOSEFU KISIMA.
SASA ENEO HILO LILIKUWA LA WASAMARIA WALIOITUMIA TORAH LAKINI HAWAKUFATIA DINI KAMA VILE WAYAHUDI.
NAHISI NJAA.
SHILINGI NI SHILINGI UWE MYAHUDI AU MSAMARIA, SIO?
TWENDE MJINI? TUONE KAMA HAWA WASAMARIA WATATUUZIA CHAKULA?
NITANGOJA HAPA NIPUMZISHE MIGUU.
TOFAUTI KATIKA DINI ILISABABISHA CHUKI NA KUTOAMINIANA KATI YA JAMII HIZI MBILI.
SAMAHANI, WAWZA KUNIPA MAJI KUTOKA KISIMA HIKI?
MIMI? WANIOMBA MIMI MSAMARIA MAJI?
UNGALIJUA ANAYEKUULIZA UNGENIULIZA MIMI NIKUPE!
NA NINGEKUPA KINYWAJI PIA. MAJI YA UZIMA.


KISIMA KIKO CHINI SANA BWANA.
HUTAPATA MAJI YOYOTE BILA JAGI NA KAMBA!
AMA WADHANI WEWE NI MZURI ZAIDI?
WADHANIA WEWE NI MKUU KAMA BABA YAKOBO ALIYENYWESHA MIFUGO NA FAMILIA YAKE NA YEYE MWENYEWE TOKA KWA KISIMA HIKI?
YAKOBO ALIKUNYWA TOKA KWA KISIMA HIKI LAKINI ALISHIKWA NA KIU TENA.
KAMA WEWE AU MIMI AMA MTU YEYOTE AYANYWAYE MAJI HAYA.
LAKINI YEYOTE AYANYWAYE MAJI YANGU YA UZIMA HATASHIKWA NA KIU TENA!
SI HIVYO TU BALI MAJI NINAYOPEANA YAWA CHEMCHEMI YENYEWE -- YAPEANA UZIMA WA MILELE!
NINGEPENDELEA HIVYO. TAFADHALI NIPE MAJI HAYA NISIWE NA HAJA YA KURUDI MAHALA HAPA TENA.
ISINILAZIMU KUTEMBEA PENYE WATU WALE NA MTAZAMO WAO . . .
ENDA NYUMBANI.
UKIJA RUDI NA MUMEO.
SI... SINA MUME.
UKWELI MTUPU.
UNA WAUME WATANO NA MUME ULIYE NAYE HIVI SASA SIO MUME WAKO
WE . . . WEWE NI NABII?


WEWE NI NABII WA KIYAHUDI, SIO?
NYINYI WAYAHUDI MWASEMA KWA KUWA TWAMUOMBA MUNGU KWA MLIMA HUU BADILI YA YERUSALEMU --
MWANAMKE WEWE . . .
BABA ATAKA WANAOMWOMBA KWA UKWELI. WANAOMWABUDU KWA ROHO NA UKWELI!
LAKINI KWENYE MLIMA HUU? YERUSALEMU? HAINA TOFAUTI.
TOFAUTI NI KUWA HUELEWI UNACHOKI-ABUDU KAMA WAYAHUDI KWA SABABU UKOMBOZI WAJA KUPITIA WAYAHUDI.
NAJUA MASIHI YUAJA NA TUTAELEWA KILA KITU ATAKAPOKUJA KUTUELEZA!
NA NIKO HAPA.
NAKUELEZA.
BWANA, MBONA WASEMA NAYE?
TUMEKULETEA CHAKULA.
NINA CHAKULA. CHAKULA USICHOKIJUA JUU YAKE.
KUNA MWENGINE ALIYEMLETEA CHAKULA?
LABDA MWANAMKE YULE?
MARAFIKI ZANGU, CHAKULA CHANGU --
-- NI KUIFANYA NIA YA ALIYENITUMA HAPA!
MKULIMA BAADA YA KUPANDA KIWANJA LAZIMA ANGOJE KUVUNA, SIO?
HAYA, FUNGUA MACHO UANGALIE KIWANJA!



YOHANA 4:4-27



NI WAKATI WA KUVUNA!
NI WAKATI WA KUVUNA KILICHOPANDWA KABLA SIJAKUJA!
-- ALIJUA KILA KITU KUNIHUSU!
VITU AMBAVYO HATA WAMBEA SANA KATI YENU HAMKUVIJUA!
SIKIZA, MUNGU NI ROHO!
NA LAZIMA WANAOMWABUDU WAMWABUDU KWA ROHO NA UKWELI!
NTAELEZEA . . .
YESU ALIKAA HAPO SIKU MBILI NA WENGI WA WATU WA SYCHAR WALIAMINI.
KISHA YESU AKAENDA ZAKE, AKAREGEA GALILAYA.
WAKATI UMEFIKA!
UFALME WA MBINGUNI UNAKARIBIA NA LAZIMA MTUBU!
TUBU NA KUAMINI!
NA HUKO ALIKARIBISHWA VIZURI NA WAGALILAYA.
ALIFUNZA KARIBU NA MJINI NA KWENYE SINAGOGI ZAO.
NA AKAFANYA ISHARA YAKE YA PILI.
BWANA!
BWANA!!!
MIMI SI AFISA WA HERODE ANTIPASI! NATOKA KAPERNAUMU!
NIMESIKIA UNACHOKIFANYA NA --
HUTAMKAMATA YESU ULIVYOMKATA YOHANA!
WAKOSA KUELEWA!


NIMESKIA JUU YAKO!
NA NILIVYOSIKIA UKO HAPA ILIBIDI NIKUONE!
MVULANA WANGU AMEKUWA MGONJWA KWA MDA MREFU NA ATAKUFA WAKATI WOWOTE SASA!
TAFADHALI NJOO UMPONYE MWANANGU!
WATAKA KUONA ISHARA NA MAAJABU NA MIUJIZA KABLA UAMINI MANENO YANGU?
TAFADHALI NJOO NAMI KABLA HAJAFA!
ANA HOMA NA HANA MDA MREFU!
ENDA NYUMBANI. MWANAO HATAKUFA.
BWANA?
ATAISHI!
NA HOMA YA KIJANA YULE IKAONDOKA ALIVYOSEMA YESU.
WAKATI YESU ALIPOSEMA.


MDA MFUPI BAADAYE YESU ALIREGEA NAZARETI.
SIKU YA SABATO ALIENDA SINAGOGI KUABUDU.
SINAGOGI ILE ILE ALIOIENDA ALIVYOKUA.
NA WATU WALE WALE ALIOABUDU NAO AKIKUA.
KARIBU YESU MWANA WA YOSEFU!
WAWEZA KUTUSOMEA KUTOKA KWA MANABII?
NDIO, BILA SHAKA.
GOMBO ALIYOPEWA ILIKUWA GOMBO YA NABII ISAYA.
"ROHO WA MUNGU YU JUU YANGU; KWA MAANA AMENITIA MAFUTA KUWAHUBIRIA MASKINI HABARI NJEMA."
"AMENITUMA KUWAFUNGA WALIOVUNJIKA MIOYO, KUWAACHA HURU WAFUNGWA NA KUWAFUNGU WALIO KAMATWA."
ILIVYOKUWA DESTURI WATU WALINGOJA.
SOMO LIKIISHA MSOMAJI ALITARAJIWA KUFUNZA KUTOKANA NALO.
MUMESIKIA NENO LA MAANDIKO.
NA LEO MAANDIKO YAMETIMIZWA MBELE YENU.
NINI?
MATHAYO 4:23-25; MARKO 1:39; LUKA 4:16-21,44


ASEMA NINI?
HUYU NI KIJANA WA YOSEFU, SIO?
JE, YWASEMA NINACHODHANIA YWASEMA?
NAJUA MWATAKA NIFANYE NILIYOFANYA KAPERNAUMU.
MWATAKA NIFANYIE KIJIJI CAHNGU NILIYOYAFANYA KWENYE SAFARI ZANGU MBALI NA NAZARETI.
LAKINI SIKIZA! NABII WA KWELI HAKUBALIWI KIJIJINI KWAO!
ELIYAH ANGETUMWA KWA WAJANE WOWOTE ISRAELI WAKATI WA KIANGAZI!
LAKINI BADALA YAKE ALITUMWA KWA MJANE WA SAREPTA KUMLISHA KIMIUJIZA!
NA ELISHA ANGETUMWA KWA MKOMAVU YEYOTE ISRAELI MDA MFUPI BAADAYE!
BADALA YAKE ALIMPONYA NAAMAN MSIRIA!
WAWEZAJE KUONGEA HIVYO!
KUTUKASHIFU HIVYO!
MUONDOE HAPA!
MTOE KIJIJINI!

LUKA 4:22-30


NABII HAWAEHESHIMIWI KWAO?
LABDA NI KWA SABABU WANATENDA BILA HESHIMA!
MPELEKE KWENYE JABALI!
MTUPE MKUFURU HUKO!
MUMTUPE HUKO -- KUNA NINI?
YUKO WAPI?
NILIKUA NIMEMSHIKILIA MIKONONI . . .
HAIWEZEKANI!
AMEENDA WAPI?
YESU?
KIVIPI --?
WAKATI UMEFIKA TUENDELEE . . .
LUKA 4:22-30


YESU ALIONDOKA NAZARETI NA BAADAYE AKAISHI KAPERNAUMU.
HATA HUKO WATU WALIMZINGIRA KUSIKIZA MAFUNDISHO YAKE.
PETRO! HUJAMBO!
PETRO? NANI? AH, KWELI . . . MIMI . . .
HUJAMBO YESU!
ULIFANIKIWA KUSHIKA WENGI JANA USIKU?
LA. KIDOGO TU . . .
KUNA . . . NAWEZA KUKUSAIDIA?
NAAM PETRO WAWEZA.
PELEKA CHOMBO KULE KIDOGO TAFADHALI.
SAWA. VYOVYOTE NAWEZA KUSAIDIA.
YESU ALIFUNZA UMATI SIKU HIYO KUTOKA KWA CHOMBO.
NA ALIVYOMALIZA . . .
PETRO ASANTE.
SASA KAMA WAWEZA KUNIFANYI KITU CHENGINE.
NIKUFANYIE NINI MWALIMU?
SIO KUNIFANYIA MIMI.




MATHAYO 4:18-22, MARKO 1:14-20, LUKA 5:1-11




MATHAYO 4:18-22, MARKO 1:14-20, LUKA 5:1-11


HATUA MBELE KIDOGO UFUONI . . .
ANDREYA WAENDA WAPI?
TWASIKIA ULISHIKA SAMAKI WENGI JANA USIKU!
LA! SASA HIVI! SIJAWAHI KUVUA WENGI NAMNA HII!
MWALIMU! ALIYAFANYA YATENDEKE!
MWALIMU.
NIMESIKIA KUHUSU MIUJIZA . . . NA MAFUNDISHO . . .
KUMFUATA MTU KAMA YEYE . . . INGEKUWA AJABU MNO . . .
NJOONI NYINYI WAWILI!
NJOO NAMI!
ENDENI!
HARAKISHA!
MTU HUYU ANA NGUVU KWA MANENO NA MATENDO!
NAO PIA WAKAMFUATA.






MARKO 1:21-28; LUKA 4:33-37




MATHAYO 8:14-17; MARKO 1:29-34; LUKA 4:38-41






MARKO 1:35-39; LUKA 4:42-44


MTU YULE ALIKUWA NA UKOMA, UGONJWA USIOPONA NA UNAOAMBUKIZA ULIOUMBUA MWILI NA KUDHURU MFUMO WA NEVA NA VIUNGO VYA NDANI.
MAISHA NA UKOMA YALIKUWA MAISHA YENYE UCHUNGU NA UPWEKE KWA SABABU KILA MTU ALIOGOPA KUAMBUKIZWA UGONJWA HUO.
BWANA . . .
. . .KAMA UNGEPENDA, TAFADHALI . . .
. . . NITAKASE!
TAFADHALI.
NINGEPENDA.
TAKATA.


NI . . .
NI . . . AH, ASANTE!
ASANTE!
HAYA NENDA!
JIONYESHE KWA MAKUHANI NA UFANYE KAFARA ZA KUJITAKASA ALIZOAMURU MUSA!
NA UHAKIKISHE HUMWAMBII YEYOTE NILIFANYA HAYA!
NAAM BWANA!
NAAM BWANA!
MTU HUYO ALIMWAMBIA KILA ALIYEKUTANA NAYE KILOCHOFANYIKA NA ALIYEKIFANYA.
HABARI IKAZIDI KUENEA.
UMESIKIA MAFUNZO YAKE SIMIONI?
NIMESKIA AKIITWA MASIHI ALIYEAHIDIWA! HATA YWASEMA HIVYO MENYEWE!
WATU HUSEMA MANENO KWA URAHISI YUDA, NI VITENDO NINA HAJA NAVYO!
KAMA KUNA WAKATI TULIHITAJI MASIHI NI SASA!
KWELI, SIMIONI.
YESU ALIPOENDA KUTOKA KIJIJI KIMOJA HADI CHENGINE UMATI ULIMFUATA.
KAMA DESTURI ALITAFUTA MAHALI KIMYA AWE PEKE YAKE NA KUOMBA.
LUKA 5:15-16


ALIVYOFUNZA KAPERNAUMU WAFUASI NA WANAKIJIJI WALIKUSANYIKA KUSIKIZA ALICHOSEMA.
LAKINI KUNDI LA WAFARISAYO NA WALIMU WA DINI KUTOKA ENEO HILI WALIKUJA KUSIKIZA PIA.
HUYU YESU ATAMPONYA VIPI RAFIKI YETU KAMA HATUWEZI KUPITA KATI YA UMATI?
NI SAWA RAFIKI ZANGU MUMEJARIBU . . .
LA!
HATUWEZI KUPITA KATI YA UMATI BASI TWENDE JUU YAKE.
KWELI -- NGOJA! NIN--?
TUTAHITAJI VIFAA.
NA KAMBA!
NINI?!?
UFALME WA MUNGU UNAKARIBIA LAKINI BABA NI MWENYE REHEMA NA ASAMEHEA.
NYINYI NANYI MUWE NA REHEMA.
NYINYI NANYI MUSAMEHE.
NA BABAB ATA --
NINI KINAENDELEA?


RAFIKI YETU ALITAKA KUKUONA YESU!
AAMINI WAWEZA KUMWANGALIA!
SASA HII NI IMANI!
RAFIKI YANGU, DHAMBI ZAKO ZIMESAMEHEWA.
AH YESU . . . ASANTE . . .
NINI?
WAWEZA KUONGEA MANENO YA KUFURU HIVYO?
HAKUNA BALI MUNGU AWEZA KUSAMEHE DHAMBI!!!
KWA NINI UNA UOVU NAMNA HIYO NDANI YAKO?
NI NINI RAHISI ZAIDI KUSEMA?
"UMESAMEHEWA DHAMBI," AU "SIMAMA UTEMBEE"?
SI . . . WAMAANISHA NINI?
ACHA NIWAONYESHE KUWA MIE, MWANA WA ADAM, NINA MAMLAKA YA KUSAMEHE DHAMBI.
SIMAMA! CHUKUA MKEKA WAKO UTEMBEE KWENDA NYUMBANI!
NI . . . NI . . . VIPI LAKINI . . .
AH, IMEKUWA MDA MREFU! ASANTE!
SITAWAHI KUISAHAU SIKU HII! JE WEWE, THOMAS?
MAAJABU!
SIJAWAHI KUONA KAMA HIVI! HUYU MTU APASWA KUFUATWA!


BAADAYE YESU ALIVYOTEMBEA KAPERNAUMU . . .
. . .HUNA TOFAUTI NA NGURUWE WA KIRUMI UNAOWAFANYIA KAZI MATHAYO LAWI!
NAJITAHIDI KWA KWELI, NAKUHAKI-KISHIA.
NAJUA WATOZA USURU WAKO WALINITOZA ZAIDI, KIDOGO CHAO KIDOGO CHAKO!
WEZI WAFANYIA WEZI --
WAANGALIA NINI?
NDIYE, SIO? YESU, MWALIMU NA TABIBU.
AH! NI MTU MTAKATIFU NA HWEZI KUTAKA LOLOTE NA MTU KAMA WEWE!
WEWE.
NIFUATE.
MIMI JE?
PESA ZANGU JE?
KUNA WATOZA USHURU WENGINE . . . WATAKUSAIDIA!
MIMI NI MATHAYO! NIMESIKIA MENGI KUMHUSU MTU HUYU!
MIMI NI MATIYA NA YOTE NI KWELI!
MIMI NI BARSABBA. TUMEMFUATA YESU KWA MDA SASA! NI JAMBO LA KUSISIMUA!


USIKU HUO MATHAYO ALIMFANYIA YESU SHEREHE.
WENGI WA WAFUASI WALIKUWEKO PAMOJA NA WATOZA USHURU WENZAKE MATHAYO.
WAFIKIRIA WAWEZA KUONDOKA TU NAMNA HIYO?
-- NAKWAMBIA YAKOBO NAJISKIA HURU!
NAYAWACHA NYUMA MAISHA HAYO KWA FURAHA!
NA TUTAENDELEA KWA NIAMBA YAKO!
NA KWA FURAHA!
NIMEWAALIKA HAPA MUKUTANE NA BWANA WANGU MPYA!
SITAFANYIA KAZI ROMA TENA!
AU PESA!
LA, NITAMFUATA HUYU, TABIBU NA MWALIMU MTAKATIFU!
MUONE!
NYINYI WAWILI MWAWEZAJE KUMFUATA ANAYEKULA NA KUNYWA NA WENYE DHAMBI KAMA WALE?
NI NANI ANAYEHITAJI TABIBU? MWENYE AFYA AU MGONJWA?
UNAJUA ANACHOMAANISHA MUNGU ASEMAPO "NATAKA REHEMA, SIO KAFARA"?
NIMEKUJA KUWAITA WENYE DHAMBI WATUBU!
HAYA VIZURI LAKINI UNAKAA HAPA UKILA NA KUNYA --
-- IJAPO SISI WAFARISAYO HUFUNGA KIDESTURI! HATA WAFUASI WA MBATIZAJI WAFUNGA!
MBONA WEWE NA WAFUASI WAKO HAMFUNGI?
JE WAGENI WA BWANA ARUSI HUMLILIA INGALI ALIPO NAO? LA!
ITAFIKA WAKATI BWANA HARUSI HATAKUWA NAO, LAKINI, KISHA WATAFUNGA.




MATHAYO 9:16-17, YOHANA 5:2-15


ASANTE! ASANTE!
USIFANYE DHAMBI TENA RAFIKI YANGU!
WAFANYA NINI?
NI SABATO! SIKU YA KUPUMZIKA!
KUBEBA MKEKA NAMNA HIYO NI HATIA KWA SHERIA YA MUNGU!
LAKINI MTU YULE ALINIAMBIA NICHUKUE MKEKA NITEMBEE! NAWEZA KUTEMBEA! NAWE --
TOSHA!
KWA NINI WAFIKIRIA WAWEZA KUFANYA VITU HIVI SIKU YA SABATO?
BABANGU AFANYA KAZI SIKU YA SABATO KWA HIYO MI PIA NAFANYA KAZI.
ANACHOFANYA BABA MWANA PIA AFANYA. HATA KUFUFUA WAFU!
JE WASEMA WEWE NI MWANA WA MUNGU? KUWA UKO SAWA NAYE?
NIKISEMA HIVYO JUU YANGU WAWEZA USIAMINI.
LAKINI YOHANA MBATIZAJI ALIONGEA KUNIHUSU.
BILA SHAKA KUNA USHUHUDA WA NGUVU ZAIDI JUU YANGU: MUNGU MWENYEWE KWENYE MAANDIKO.
LAKINI MWAKATAA KUONA.
BADALA YAKE MNASOMA MAANDIKO KUWAKASHIFU WENGINE NA SHEIA HIYO HIYO INAWAKASHIFU NYINYI WENYEWE!
MWASEMA MWAMWAMINI MUSA LAKINI KAMA INGELIKUWA UKWELI MNGELINIAMINI MIMI.
ALIANDIKA JUU YANGU!
LAKINI VILE HAMWAMINI MAANDIKO YAKE MTANIAMINI VIPI?





MATHAYO 12:1-14; MARKO 2:23-28; MARKO 3:1-6; LUKA 6:1-11


AKIYAJUA HAYA YESU AKAONDOKA.
HAYA YOTE YALITIMIZA ALIYOSEMA ISAIYA JUU YA MASIHI:
"TAZAMA KIJAKAZI WANGU NILIYEMCHAGUA. MPENDWA AMBAYE NDANI YAKE ROHO YANGU IMERIDHIKA. NIMEWEKA ROHO YANGU KWAKE YEYE . . .NA KWENYE JINA LAKE MATAIFA YOTE HATA WAYUNANI WATAWEKA IMANI YAO."
NA SIKU MOJA BAADA YA KUOMBA PEKE YAKE KWENYE MLIMA USIKU MZIMA YESU ALIWACHAGUA WANAUME KUMI NA WAWILI KUTOKA WAFUASI WAKE.
SIMIONI ALIYEITWA PETRO.
ANDREYA KAKAKE PETRO.
YAKOBO --
NA YOHANA MWANA WA ZEBEDAYO.
FILIPO.
NATHANELIWA CANA ALIYEITWA BARTOLOMAYO.
TOMASO ALIYEITWA INAYOMAANISHA "PACHA".
MATHAYO ALIYEITWA LAWI MTOZA USHURU.
YAKOBO "MDOGO"
SIMIONI MKANANAYO.
YUDA AMBAYE ANGEJULIKANA BAADAYE KAMA THADAYO.
YUDA ISKARIOTE.
WAUME HAWA WALIITWA MITUME NA WALIPEWA MAMLAKA YA KUHUBIRI NA KUPONYA NA KUTOA MIZIMWI.
MATHAYO 10:1-4; MARK 3:13-19; LUKA 6:13-16





# HADITHI YA MKE WA MVUVI

## "UVUVI MKUU"




ANGEWACHAJE SAMAKI WENGI ALIOWAHI KUWASHIKA?
HASA WAKATI MAMANGU AUGUA SANA . . .
UKO SAWA MAMA?
NDIO MPENZI, ASANTE.
SIMIONI!
HUKUJA NYUMBANI! NILIDHANI UMEUMIA AU UMEKUFA!
KISHA NAGUNDUA UMEACHA SAMAKI WENGI ZAIDI ULIOWAHI KUWASHIKA...
JAMAA WAKISHUGHULIKIA. WATAKULETEA PATO LANGU...
WADHANI NI PESA NINA WASIWASI NAZO?
WAMFUATA YULE MWALIMU MPYA ANAYEDAI YEYE NI MASIHI!
NDIO.
ANAYESEMA HIVYO KUJIHUSU AIDHA ANA KICHAA AU ADANGANYA AMA YOTE MAWILI!
LA. MTU HUYU NI MKARIMU NA MWENYE HEKIMA, HANA KICHAA.
NA SIDHANI AWEZA KUDANGANYA HATA KWA KUPENDA. LAKINI NAJUA HANGEPENDA.
SIMIONI ALIELEZA KILA KITU. KWA NINI YEYE NA ANDREYA NA YAKOBO NA YOHANA NA WENGINE WENGI WALIMFUATA HUYU YESU.
ALINIAMBIA KUHUSU MAFUNZO NA MIUJIZA.
NA KWA MARA NYENGINE NILIMUAGA MUME WANGU KWAHERI ALIPOONDOKA --
TAFADHALI SIMIONI USI --
LAZIMA.
NIKIWAZA KAMA NINGEWAHI KUMUONA TENA.


SABATO ILIFIKA KABLA HAJAREGEA.
MAMA. HUJAKUWA UKILA VIZURI.
SIJAKUWA NA NJAA --
WAGENI! UNA WAGENI!
HUJAMBO MPENZI.
SIMIONI?
NIMELETA MGENI.
SIKO TAYARI KUPOKEA WAGENI...
INGIA! INGIA! KWA HIYO WEWE NDIO YESU ANAYEMZUNGUMZIA SIMIONI!
PETRO ALINIAMBIA MAMAKO BADO AUGUA.
NAWEZA KUMUONA?
MNAKIJUA KILICHOTENDEKA BAADAYE.
YWAWEZA?
ANGALIA TU.
ACHA NIKUPE CHAKULA!
LAZIMA UNA NJAA! MI NINA NJAA!



BAADA YA HIVYO?
SASA WAELEWA MPENZI?
ALINIALIKA KUWA MVUVI WA WATU.
KUNA JAMBO MOJA TU LA KUFANYA --
-- PETRO
USIKU HUO YESU ALIWAPONYA WENGI, WENGI WALIOKUJA KWETU.
ASUBUHI --
-- NILIMUAGA MUME WANGU TENA.
MKE WA MVUVI AMBAYE MUMEO SASA ALIVUA KITU TOFAUTI.
UVUVI MKUU.

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."





SUPERBIBLE.TV